Shiriki Hadithi yako

- Shirikiana na wanaoshughulika na kesi na uwape majina na taarifa ya kuwasiliana ya watu wambao wanaweza to taarifa zaidi. Katika matukio mengine, kauli ya maandishi inaweza hitajika.
- Ambavyo wanaoshughulika na kesi yako watakuwa na taarifa ndivyo watakavyo fanya uamuzi vizuri.

Majukumu ya Wazazi

- Hakikisha umewapeleka watoto wako kuhudhuria miadi yoyote au mtaalamu itakapohitajika.
- Hakiki anayeshughulika na kesi yako anajua mabadiliko yoyote, kama vile anwani na nambari ya simu mpya au mtu mgeni anayeishi nyumbani kwako.
- Hudhuria mikutano yote iliyopangwa kuhusu kesi yako ya watoto au vijana wako.

Ufikiaji wa Rasilimali Zinazopatikana

- Uliza maswali kuhusu mchakato na hatua unazohitajika kuchukua.
- Uliza kuhusu rasilimali zinazopatikana. Katika nchi zingine, mawakili wa wazazi wanaweza kukusaidia wakati wa uchunguzi.

Anwani za mawasiliano

Kwa maswali au masuala kuhusu kesi yako: Wasiliana na mshughulikiaji wa kesi au msimamizi wao.

Ikiwa hauna uhakiki wa nani unapaswa kuwasiliana naye, tafuta ofisi yako ya mtaa na uombe kuzungumza na mtu kuhusu kesi yako katika **https://apps-ca-ext.dcyf.wa.gov/CAOfficesPub/offices/general/OfficePick.asp**

Mahusiano ya Wananchi

Hutoa mchakato wa kutatua malalamishi yanayohusiana na ulinzi wa watoto na ustawi, nyumbani kwa kulelea watoto na leseni ya uangalizi wa watoto, programu za uangalizi wa watoto na huduma za urekebishaji wa watoto.

Nambari ya simu: (360) 902-8060 au 1-800-723-4831
Barua pepe: constrelations@dcyf.wa.gov
www.dcyf.wa.gov/contact-us/constituent-relations

Office of the Family and Children's Ombuds (Ofisi ya Mchunguzaji wa Familia na Watoto, OFCO)

Mtu yeyote anaweza wasilianana na OFCO ikiwa ana malalamishi au ameshindwa kutatua malalamishi na DCYF. OFCO ni ofisi huru iliyomo ndani ya Ofisi ya Gavana.

Nambari ya Simu: (206) 439-3870 au (800) 571-7321
https://ofco.wa.gov

Programu ya Ufikiaji wa Huduma na Haki za Raia

Pata maelezo zaidi kwa **www.dcyf.wa.gov/service-access**

---

*Ikiwa ungetaka nakala bila malipo za chapisho hili kwa muundo mwingine au ligha, tafadhali wasiliana na Mahusiano ya Wananchi DCYF kwa 1-800-723-4831 au barua pepe kwa **communications@dcyf.wa.gov**.*

DCYF PUBLICATION CWP_0083 SI (12-2025) Swahili

UCHUNGUZI:

Njia ya huduma za ulinzi wa watoto (CPS) ya kuchunguza unyanyasaji au utelekezaji wa watoto na vijana

Washington State Department of
CHILDREN, YOUTH & FAMILIES

Je, Uchunguzaji wa Child Protective Services (Huduma za Ulinzi wa Watoto, CPS) ni nini?

Uchunguzaji wa CPS hufanyika wakati mtu ataripoti kuwa mtoto au kijana anaweza kuwa amenyanyaswa au ametelekezwa. Mshughulikiaji wa kesi wa DCYF hufuatilia hali ili kujua nini kilichofanyika, ikiwa mtoto au kijana yuko salama kwa sasa na ikiwa kuna hatari ya madhara siku zijazo.

Mshughulikiaji kesi huongea na watoto, vijana, wazazi au waangalizi wa watoto na watu wengine ambao wanaweza kuwa na taarifa muhimu. Lengo ni kuelewa ukweli na kuhakikisha kuwa watoto na vijana wamelindwa.

Je, mbona napokea uchunguzi huu?

- Department of Children, Youth & Families (Idara ya Watoto, Vijana na Familia wa Jimbo, DCYF) ilipokea ripoti ya masuala kuhusu usalama wa watoto na vijana walio nyumbani kwako.
- Ripoti hiyo ilikimu ufafanuzi wa kisheria wa unyanyasaji na utelekezaji (RCW 26.44.020).
- Ripoti hiyo ilionyesha mashtaka yalikuwa hatari kwa wastani au hatari zaidi au kunaweza kuwa na hatari ya hivi karibuni ya mtoto au kijana wako.
- DCYF inataka kushirikiana nawe ili kuhakikisha kuwa mtoto au kijana wako yuko salama.

Changanua msimbo wa QR au utembelee: **https://apps.leg.wa.gov/WAC/default.aspx?cite=110-30&full=true** ili kupata ufafanuzi wa unyanyasaji na utelekezaji.

Unachopaswa kutarajia kutoka kwa uchunguzi

- Lengo la DCYF nikuleta familia pamoja wakati ni salama kufanya hivyo. Mshughulikiaji wa kesi atafanya kazi nawe ili kupata mbinu za kuweka mtoto/kijana salama akiwa nyumbana ikiwa itawezekana.
- Wewe na mtoto/kijana wako mnafaa kushughulikiwa kwa usawa na kwa heshima wakati wote wa mchakato huu.
- Mshughulikiaji kesi wa DCYF atakuja nyumbani kwako ili aweze kuelewa vyema hali yako.
- Utahojiwa kama ilivyo sehemu ya uchunguzi. Hii inajumuisha wazazi, walezi au mtu yeyote ambaye ametajwa katika ripoti hii.
- Watoto au vijana wanaweza kuhojiwa pia na kupigwa picha kama ilivyo sehemu ya uchunguzi. Hili linaweza fanyika bila ruhusa yako, kama ilivyoruhusiwa na sheria. Watoto au vijana wako na haki ya kuagiza mtu mzima wa kuaminika atakaye kuwa naye wakati wa uchunguzi huu. Uliza mshughulikiaji kesi wako ambaye anarejelewa kama mtu mzima anayetegemewa.
- Mshughulikiaji kesi wa DCYF atakusanya kuwa kuhakiki rekodi na kuzungumza na watu wanajua mtoto wako, kijana au familia- watu kama walimu, madaktari au wanajamii.
- Wataalamu tofauti wanweza hitaji kufanya kazi pamoja ili kusaidia usalama au ustawi wa mtoto wako au vijana wako. Hii inaweza jumuisha polisi wa mtaa wako na vituo vya utetezi wa watoto n.k
- Huduma za usaidizi zinaweza kutolewa ili kusaidia familia kukaa kwa usalama na yenya afya.

Je, kesi "kukubalika" na "kukataliwa" inamaanisha nini?

Baada ya uchunguzi, DCYF itaamua ikiwa kesi imekubalika au imekataliwa.

- **Kesi kukubalika** ni kumaanisha kulikuwa na taarifa ya kutosha ya kuonyesha kuwa kuna uwezakano wa unyanyasaji au utelekezaji ulifanyika.
- **Kesi kukataliwa**ni kumaanisha kuwa hakukuwa na taarifa ya kutosha ya kuonyesha kuwa unyanyasaji au utelelekezaki ulifayika.

Je, niatelezwa aje kuhusu matokeo?

Unaweza kujulishwa ana kwa ana, kupitia simu au kupitia barua pepe. Barua pia itatumwa kwa anwani yako ya nyumbani. Ikiwa matokeo yataonyesha kesi imekubalika, barua hiyo itajumuisha maagizo ya jinsi ya kukataa rufaa.

Una siku 30 kuanzia tarehe utakayopokea barua hii ili utume rufaa yako. Ikiwa utahama, hakikisha kuwa mtu anayeshughulika na kesi yako anajuwa anwani yako mpya ili usikose kupokea barua muhimu.

Je, ikiwa mashtaka yatakubalika yataniadhiri kivipi?

Mashataka yatakayokubalika yanaweza kutumika katika hali mahususi kama:

- Ushahidi katika kesi kortini kuhusu watoto wako.
- Wakati wa kuamua ikiwa unaweza fanya kazi, kujitolea au kupata leseni ya uangalizi wa watoto au watu wazima ambao hawako katika hali ya usalama.
- Kama taarifa ya msingi ikiwa kuna ripoti za siku zijazo.

Certificate of Parental Improvement (Cheti cha uboreshaji wa Uzazi, CPI) hutoa kizuizi cha watu walio na mashtaka yaliyokubalika ya unyanyasaji au etelekezaji wanapotuma ombi la kufanya kazi katika kituo cha usaidizi wa kuishi au makao ya uangalizi wa wazee, kutoa husuma za muda mrefu za uangalizi au kuomba ufikiaji ambao hausimamiliwi chini ya programu ya DCYF.

Tembela **www.dcyf.wa.gov/safety/can-founded-findings/cpi** ili kupata maelezo zaidi.